WCF
Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

# FIDIA eNEWSLETTER

TOLEO LA APRILI - JUNI 2026 | www.wcf.go.tz




## MAMIA YA WANANCHI WAPATA ELIMU YA FIDIA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA

Karibu Sana

WCF Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

# YALIYOMO:


- Waziri Sangu Awataka Waajiri Kuzingatia Sheria za Kazi
- WCF Yatoa Elimu kwa Wachimbaji Wadogo wa Madini Mirerani
- WCF Yaendelea Kuunga Mkono Dhamira ya Serikali Kulinda Haki za Wafanyakazi
- WCF Yashiriki Mjadala wa Kitaaluma wa Chama cha Waajiri
- Mamia ya Wananchi Wapata Elimu ya Fidia wiki ya Utumishi wa Umma


Jarida Mtandaoni
Skani Kodi ya QR
Hapo Chini


TIMU YA WAHARIRI

MWENYEKITI
Dkt. John K. Mduma

MHARIRI MKUU
Laura G. Kunenge

MHARIRI MSAIDIZI
Sophia F. Mtakasimba

WACHANGIAJI
Mcharo S. Mrutu
Meseka Z. Kadala
Lilian R. Shembilu
Nuru A. Mwakivuma

# DIBAJI




Ni furaha kubwa kukukaribisha katika Jarida la Robo ya Nne la Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF). Toleo hili linaendelea kuakisi dhamira ya Mfuko ya kuwahudumia wadau wake kwa ufanisi huku likitoa taarifa kuhusu shughuli mbalimbali zilizotekelezwa katika kipindi hiki.

Katika toleo hili, utabaini kuwa sehemu kubwa ya habari zimejikita katika utoaji wa elimu kwa umma. Hili si jambo la bahati mbaya, bali ni utekelezaji wa moja ya vipaumbele vikuu vya Mfuko. WCF inaamini kuwa utoaji wa elimu endelevu kwa waajiri, wafanyakazi na wananchi kwa ujumla ni nguzo muhimu katika kuhakikisha wadau wanaelewa wajibu na haki zao chini ya mfumo wa fidia kwa wafanyakazi.

Kupitia elimu hiyo, waajiri wanaendelea kuhamasishwa kutimiza wajibu wao wa kuwasajili wafanyakazi na kuwasilisha michango kwa wakati, huku wafanyakazi wakijengewa uelewa kuhusu haki zao wanapopata madhila yatokanayo na kazi. Aidha, elimu hii huchangia kuongeza uelewa kuhusu taratibu za kuwasilisha madai ya fidia na huduma mbalimbali zinazotolewa na Mfuko.

Katika kipindi hiki, WCF imeendelea kuwafikia wadau kupitia maonyesho ya kitaifa, mikutano na semina, programu za uhamasishaji, vyombo vya habari na majukwaa ya kidijitali. Jitihada hizi zina lengo la kuhakikisha taarifa sahihi zinawafikia wananchi wengi zaidi.

Tunatoa shukrani za dhati kwa wadau wetu wote kwa ushirikiano wanaoendelea kuupatia Mfuko katika kutekeleza majukumu yake. Ushirikiano huo unatupa nguvu ya kuendelea kuboresha huduma na kuwafikia Watanzania wengi zaidi kupitia elimu na mawasiliano yenye tija.

Tunakuomba uendelee kuwa balozi wa elimu hii kwa kushiriki maarifa utakayoyapata katika toleo hili na kuwafikishia wengine. Kwa pamoja, tunaweza kujenga jamii yenye uelewa mpana kuhusu huduma za fidia kwa wafanyakazi.

**Dkt. John Mduma**

Mkurugenzi Mkuu

# WAZIRI SANGU AWATAKA WAAJIRI KUZINGATIA SHERIA ZA KAZI




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Deus Sangu (Wa pili kutoka kulia) akiwa na baadhi ya viongozi wa WCF na Viongozi wa Kiwanda cha Nyanza Bottling Company katika ziara ya kufuatilia utekelezaji wa sheria ya ajira na mahusiano kazini.*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Deus Sangu, amewasisitiza waajiri nchini juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria za kazi, ikiwemo kuwasilisha michango ya wafanyakazi katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa lengo la kulinda maslahi ya wafanyakazi dhidi ya madhila yanayotokana na kazi.

Mhe. Sangu ametoa rai hiyo wakati wa ziara yake ya kikazi katika Viwanda vya Ziwa Steel na Nyanza Bottling Company vilivyopo Jijini Mwanza, ambapo alijionea utekelezaji wa sheria za kazi na ustawi wa wafanyakazi katika maeneo hayo.

“Serikali imeendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa sheria za kazi ili kuhakikisha wafanyakazi wanapata haki zao stahiki na wanafanya kazi katika mazingira salama, yenye tija na yanayozingatia utu wa mfanyakazi,” alisema Mhe. Sangu.
Waziri Sangu pia amewahimiza waajiri wote nchini kuhakikisha wanatoa mikataba ya ajira kwa wafanyakazi wao, kuwasajili katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) pamoja na kuwasilisha michango yao kwa wakati ili kulinda maslahi yao ya sasa na baadaye.

Ziara ya hiyo Waziri Sangu ni sehemu ya juhudi za Serikali za kufuatilia utekelezaji wa sheria za kazi, kuimarisha mahusiano mema kati ya waajiri na wafanyakazi na kuhakikisha haki, usalama na ustawi wa wafanyakazi vinaendelea kulindwa katika sekta mbalimbali za uzalishaji nchini.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. Said Mtanda, alisisitiza umuhimu wa WCF kuendelea kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi ili kuongeza uelewa kuhusu haki, wajibu na manufaa yanayotolewa kupitia mfumo wa fidia kwa wafanyakazi.

Mhe. Mtanda alisema hayo alipokutana na viongozi wa WCF waliomtembelea ofisini kwake kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na kupeana mrejesho kuhusu utekelezaji wa kazi za WCF, ambapo aliongeza kuwa huduma za fidia kwa wafanyakazi zinazotolewa katika mkoa huo zimekuwa msaada muhimu kwa wafanyakazi na familia zao pale wanapokumbwa na madhila yatokanayo na kazi.

Katika kikao hicho, Mkurugenzi wa Fedha, Mipango na Uwekezaji WCF, Bw. Bezil Ewala, alimueleza Mhe. Mkuu wa Mkoa kuhusu majukumu na huduma mbalimbali zinazotolewa na WCF, pamoja na hatua zinazochukuliwa kuhakikisha wafanyakazi wanaopata magonjwa au ajali zitokanazo na kazi wanapata stahiki zao za matibabu na fidia kwa mujibu wa sheria.

Ziara hiyo ya Uongozi wa WCF ilikuwa ni sehemu ya juhudi za Mfuko kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali katika kuhakikisha huduma za fidia kwa wafanyakazi zinawafikia walengwa.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano, Mhe. Deus Sangu (Kushoto) akipokea maelezo kuhusu namna kiwanda cha Nyanza Bottling Company kinavyozingatia sheria ya ajira na mahusiano kazini kutoka kwa mwakilishi wa kiwanda hicho.*




*Waziri Sangu, pamoja na baadhi ya viongozi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) wakipata maelezo kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini kutoka kwa mwakilishi wa kiwanda cha Nyanza Bottling Company.*




*Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Said Mtanda (Katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa WCF waliokuwa wamemtembelea ofisini kwake.*

# WCF YATOA ELIMU KWA WACHIMBAJI WADOGO WA MADINI MIRERANI




*Meneja wa Tathmini Vihatarishi Mahali pa Kazi wa WCF, Bi. Naanjela Msangi akizungumza wakati wa tukio la kutoa elimu na msaada kwa wachimbaji wadogo wa madini Mirerani, Mkoani Manyara.*

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umetoa elimu kuhusu namna ya kujikinga na ajali na magonjwa yanayotokana na kazi kwa wamiliki na wachimbaji wadogo wadogo wa madini Mirerani Mkoani Manyara pamoja na msaada wa vifaa kinga dhidi ya magonjwa kwa wachimbaji hao.

Zoezi hilo la kutoa elimu pamoja na kugawa msaada wa vifaa kinga liliongozwa na Meneja wa Tathmini Vihatarishi Mahali pa Kazi wa WCF, Bi. Naanjela Msangi, ambaye alimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa WCF, tukio lilihudhuriwa pia na maafisa kutoka Ofisi ya Madini mkoani Manyara pamoja na uongozi wa Chama cha Wachimbaji Wadogo wa eneo hilo (MAREMA).

**Akizungumza wakati wa tukio hilo Bi. Msangi alisema kuwa Mfuko umefikia uamuzi wa kuwafikia wamiliki na wachimbaji wadogo wa madini ili kuwafahamisha kuhusu huduma zinazotolewa na WCF na umuhimu wa kuchukua tahadhari ya ajali na magonjwa yanayotokana na kazi kutokana na kutambua mchango wao katika ukuaji wa uchumi wa Taifa hasa ikizingatiwa kwamba kundi hilo ni sehemu ya nguvu kazi muhimu ya Taifa.**

“Sote tunafahamu kwamba shughuli za uchimbaji mdogo wa madini hususani katika eneo hili la Mirerani zina mchango mkubwa katika kuongeza ajira na ukuaji wa Uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo, mtakubaliana nami kuwa wachimbaji hawa wanaendelea kukabiliwa na hatari nyingi za kazi, ikiwa ni pamoja na vihatarishi kwa afya zao. Hatari hizi huchangia ajali na magonjwa kama vile kifua kikuu yanayoweza kupelekea vifo kwa wachimbaji. Sasa, pamoja na mambo mengine muhimu, WCF tuna wajibu wa kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu njia bora za kujilinda au kuepukana na vihatarishi vya ajali au magonjwa yanayotokana na kazi, ndio maana leo hii tupo hapa ikiwa ni sehemu ya kutekeleza jukumu hili,” alisema Bi. Msangi.

*Afisa Tathmini Mwandamizi kutoka WCF Dkt. Kyangwe Wambura akitoa elimu kuhusu shughuli za WCF kwa wachimbaji wadogo wa Madini Mirerani*



Kwa upande wa viongozi wa MAREMA mkoa wa Manyara waliishukuru Serikali kwa kujali afya za makundi mbalimbali katika jamii ambayo yana mchango mkubwa katika ukuaji wa Uchumi wa Taifa, na kuahidi kutoa ushirikiano kwa WCF kuendeleza elimu kuhusu fidia kwa wafanyakazi wa wachimbaji wadogo waliopo katika migodi mbalimbali nchini.

“Kwanza niishukuru sana Serikali kupitia WCF kwa kujali afya zetu kutokana na mazingira yetu tunayofanyia kazi. Sisi wachimbaji mazingira yetu ya kazi ni hatarishi ambayo yamekuwa yakizalisha ulemavu na magonjwa mbalimbali. Hivyo, sisi tumeupokea msaada huu kwa matumaini makubwa tukiamini kwamba huko mbele ya safari Serikali itaangalia namna ambavyo wachimbaji wadogo wanaweza kuingizwa rasmi katika utaratibu wa WCF,” alisema Bw. Tariq James ambaye ni Katibu wa MAREMA mkoa wa Manyara.

“Mtaji wa mtu ni afya njema. Hivyo WCF ni taasisi imekuja kuokoa maisha ya wafanyakazi na tuzidi kuomba Mungu kwamba huko mbele ya safari Serikali iweke utaratibu utakaotuwezesha na sisi wachimbaji wadogo tuwe ni wanufaika wakubwa wa Mfuko huu”, alisema Bi. Rachael Njau ambaye ni Katibu wa MAREMA tawi la Mirerani.

Kupitia zoezi hilo WCF iliweza kufikia jumla ya vitalu vitano vya wachimbaji wadogo na kugawa vifaa kinga vitakavyosaidia kudhibiti magonjwa na hatari mbalimbali zinazoweza kusababishwa na shughuli za uchimbaji.

*Meneja wa Tathmini Vihatarishi Mahali pa Kazi wa WCF, Bi. Naanjela Msangi akikabidhi msaada wa vifaa kinga kwa uongozi wa Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Madini Mirerani (MEREMA).*











# WCF YAENDELEA KUUNGA MKONO DHAMIRA YA SERIKALI KULINDA HAKI ZA WAFANYAKAZI




*Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo.*

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeendelea kuunga mkono dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha haki za wafanyakazi zinalindwa.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, wakati akifungua kikao kazi cha Maafisa Rasilimali Watu na Utawala pamoja na Maafisa wa Afya na Usalama kutoka mikoa mbalimbali Tanzania, kilichofanyika hivi karibuni mkoani Singida.

Amesema mafunzo hayo ni sehemu ya mkakati wa WCF wa kuwajengea uwezo wadau mbalimbali ili kuongeza uelewa kuhusu huduma zinazotolewa na mfuko, sheria ya fidia kwa wafanyakazi, na mifumo ya kidijitali inayotumika katika kushughulikia ajali na magonjwa.

"Tunapowekeza katika elimu ya fidia kwa wafanyakazi tunalinda nguvu kazi ya taifa na kuongeza tija katika uzalishaji, ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanauelewa wa kutosha kuhusu masuala ya fidia." Amesema Dkt. Mduma

Aidha amewataka washiriki kutumia mifumo ya kidijitali ya WCF ili kurahisisha utoaji wa huduma na kuongeza ufanisi kwa waajiri na wafanyakazi nchini kote.

Amewataka washiriki kutumia mafunzo hayo kama chachu ya mabadiliko katika taasisi zao kwa kuzingatia kanuni za usalama na afya mahali pa kazi. Amesisitiza kuwa kupunguza ajali na magonjwa yatokanayo na kazi kutasaidia kuongeza ustawi wa wafanyakazi na kuchochea maendeleo endelevu ya uchumi wa Taifa.

Mmoja wa washiriki wa kikao kazi hicho, Bi. Neema Msuya kutoka Wilaya ya Iramba, alisema mafunzo hayo yamekuwa na manufaa makubwa katika kuwaongezea uelewa kuhusu masuala ya fidia na taratibu za kuwasilisha madai ya wafanyakazi.

“Tumepata elimu muhimu kuhusu namna ya kushughulikia ajali kazini na kutumia mifumo ya kidijitali ya WCF. Hii itatusaidia kutoa huduma bora zaidi kwa wafanyakazi katika taasisi zetu,” alisema Bi. Msuya.




*Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya washiriki.*

Jumla ya washiriki 160 kutoka katika Mikoa ya Singida, Njombe, Tabora na Mwanza walishiriki mafunzo hayo ya siku mbili ambapo mada mbalimbali zilikilishwa ikiwemo usalama na afya mahala pa kazi, taratibu za kuwasilisha madai, mfumo ya kidijitali pamoja ya sheria ya fidia kwa wafanyakazi.

***Baadhi ya watoa mada na washiri katika mafunzo***














# WCF YASHIRIKI MJADALA WA KITAALUMA WA CHAMA CHA WAAJIRI




*Mkuu wa Kitengo cha Takwimu na Hadhari wa WCF, Bw. James Tenga akiwa na wanajopo wengine wakati wa mjadala wa kitaaluma uliandaliwa na ATE*

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeshiriki katika mjadala wa kitaaluma ulioandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), uliobeba mada isemayo, "Kuimarisha Hifadhi ya Jamii na Uendelevu wa Biashara kupitia Ushirikiano wa Kimkakati, Ufanisi wa Mifumo ya Udhibiti na Ushirikiano wa Taasisi."

Mjadala huo umefanyika tarehe 25 Juni 2026 jijini Dar es Salaam, wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Waajiri ulioambatana na Kongamano la Waajiri, ukijumuisha wadau mbalimbali kutoka sekta ya ajira, hifadhi ya jamii na taasisi nyingine muhimu.

Akichangia katika mjadala huo, Mkuu wa Kitengo cha Takwimu na Hadhari wa WCF, Bw. James Tenga, ameelezea umuhimu wa kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii kwa kuweka nguvu kwenye matumizi ya teknolojia na miradi ya kimkakati kama Jamiinamba.

Aidha, alibainisha kuwa, tukiweza kushirikiana na kutumia mifumo hii vizuri, itasaidia kupanua wigo wa wanachama, kuongeza fursa za ajira, na kuleta tija pamoja na ukuaji wa kiuchumi kwa mifuko ya hifadhi, waajiri na wafanyakazi kwa ujumla.

Ushiriki wa WCF katika kongamano hilo umeendelea kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za hifadhi ya jamii, waajiri na wadau wengine muhimu, kwa lengo la kukuza mazingira bora ya kazi, kuimarisha ulinzi wa wafanyakazi, na kuhakikisha uendelevu wa shughuli rasmi za biashara nchini.

# MAMIA YA WANANCHI WAPATA ELIMU YA FIDIA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA

Zaidi ya wananchi 850 walitokeza kupata elimu kuhusu huduma Fidia kwa wafanyakazi kutoka Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika kuanzia tarehe 16 hadi 23 Juni 2026 katika Viwanja vya Chinangali, jijini Dodoma.

Katika maadhimisho hayo, jopo la wataalamu wa WCF lililoongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Rasilimali Watu na Utawala, Bw. Festo Kandonga, lilitoa elimu kwa wananchi waliotembelea banda la Mfuko kuhusu majukumu ya WCF, umuhimu wa usajili wa waajiri, haki za wafanyakazi wanaopatwa na madhila yatokanayo na kazi pamoja na taratibu za kuwasilisha madai ya fidia. Wananchi pia walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata ufafanuzi kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Mfuko.

Akizungumza wakati wa maadhimisho hayo, Bw. Kandonga alisema ushiriki wa WCF katika Wiki ya Utumishi wa Umma ni sehemu ya mkakati wa Mfuko wa kuendelea kutoa elimu kwa umma ili kuongeza uelewa kuhusu huduma zake na kuhakikisha waajiri na wafanyakazi wanazifahamu haki na wajibu wao kwa mujibu wa sheria. Alibainisha kuwa utoaji wa elimu unaendelea kuwa moja ya vipaumbele vya Mfuko katika kuboresha huduma kwa wananchi.

Mbali na kutoa elimu, WCF ilijibu maswali mbalimbali kuhusu fidia kwa wafanyakazi. Ushiriki huo uliwezesha wananchi wengi kupata taarifa sahihi kuhusu huduma za Mfuko na kuimarisha mahusiano kati ya WCF na wadau wake.



***Pichani: Wananchi na wageni mbalimbali wakipata elimu katika Banda la WCF wakati wa Wiki ya Utumishi wa Umma***












# HABARI KATIKA PICHA WAKATI WA SHEREHE ZA MEIMOSI 2026














Baadhi ya Wafanyakazi wa WCF waliohudhuria Maadhimisho ya Sherehe za Meimosi 2026








# WCF YANG'ARA MAONESHO YA AFYA NA USALAMA MAHALI PA KAZI

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeibuka mshindi katika Maonesho ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSH) yaliyofanyika mkoani Njombe Aprili 23-24 mwaka huu, kufuatia kutambuliwa kwa ubora wake katika utoaji wa elimu na huduma zinazolenga kuimarisha usalama na ustawi wa wafanyakazi nchini.

Tuzo hiyo ilikabidhiwa wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, ambapo taasisi mbalimbali zilishiriki kuonesha huduma, bidhaa na ubunifu unaochangia kuimarisha afya na usalama wa wafanyakazi. WCF ilitumia maonesho hayo kutoa elimu kuhusu sheria, huduma za fidia kwa wafanyakazi wanaopata madhara yatokanayo na kazi, pamoja na wajibu wa waajiri kujiandikisha na kuchangia Mfuko.

Katika kipindi chote cha maonesho, wataalamu wa WCF walitoa ushauri na elimu kwa waajiri, wafanyakazi na wananchi kuhusu namna ya kuzuia ajali na magonjwa yatokanayo na kazi, umuhimu wa kuripoti ajali kwa wakati, pamoja na taratibu za kupata fidia kwa mujibu wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo kwa niaba ya Mfuko, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano WCF, Bi. Laura Kunenge alisema ushindi huo ni matokeo ya juhudi za taasisi katika kuendelea kuboresha huduma kwa wadau na kuwekeza katika utoaji wa elimu kwa umma kuhusu haki na wajibu unaohusu fidia kwa wafanyakazi. Alibainisha kuwa WCF itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa elimu ya afya na usalama mahali pa kazi.














Ushindi huo unamaanisha nafasi ya WCF kama taasisi muhimu katika kuhamasisha mazingira salama ya kazi na kulinda ustawi wa wafanyakazi nchini. Aidha, tuzo hiyo ni chachu ya kuendelea kuboresha huduma, kuongeza uelewa kwa wadau na kuunga mkono jitihada za Serikali za kuhakikisha kila mfanyakazi anafanya kazi katika mazingira salama na yenye staha.

**TANGAZO**

# TARATIBU ZA KUWASILISHA MADAI

**(Kwa Mujibu wa Kifungu cha 77 - Employee Rights Notice)**

Kulingana na matakwa ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura 263 [marejeo ya mwaka 2015], mfanyakazi anayo haki ya kupata fidia endapo atapata ajali, ugonjwa au kifo kinachotokana na kazi.



## 1.0 AJALI

Ajali inamaanisha ajali inayotokana na kazi na kumpelekea mwajiriwa kupata majeraha.
Ajali zinazoshughulikiwa chini ya Sheria ya WCF ni zile zinazotokea katika eneo la mwajiri wakati mfanyakazi akitimiza majukumu yake ya kazi.
Ajali zinazotokea barabarani zinazohusisha chombo cha moto wakati mfanyakazi akiwa njiani anarudi/ anaenda kazini na mfanyakazi akiwa katika kazi maalumu na ajali zinazotokea barabarani zisizohusisha chombo cha moto wakati mfanyakazi akiwa njiani anarudi/ anaenda kazini na mfanyakazi akiwa katika kazi maalumu.

## 2.0 UGONJWA

Ugonjwa unamaanisha magonjwa yaliyotajwa kwenye jedwali la tatu katika Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi [Sura ya 263] au ugonjwa wowote uliotokana na kazi.

## 3.0 KIFO

Kifo kitakachosababishwa na ajali kazini au ugonjwa unaotokana na kazi.

## 4.0 HAKI YA MATIBABU

Mfanyakazi aliyepata ajali inayotokana na kazi anastahili kupatiwa huduma ya matibabu moja kwa moja chini ya utaratibu wa WCF. Huduma ya matibabu inahusisha uchunguzi, dawa, huduma za kitabibu na rufaa ya matibabu pale inapohitajika. Aidha, WCF itatoa kibali cha matibabu ya Ugonjwa baada ya kujiridhisha kama ugonjwa ulioripotiwa unatokana na kazi.

## 5.0 HAKI YA FIDIA

Mfanyakazi atakayepata ajali au ugonjwa unaotokana na kazi anastahili fidia zifuatazo;

a) Ulemavu wa Muda.
b) Ulemavu wa kudumu na kupoteza uwezo wa kufanya kazi kwa kiwango kilichothibitishwa kitabibu.
c) Huduma ya Utengemao kwa lengo la kumsaidia kuweza kurudi kazini haraka na kushiriki katika shughuli nyingine za kijamii ambazo zitamuingizia kipato na
d) Malipo kwa anayemhudumia mgonjwa ambaye amepata ulemavu wa kudumu unaomfanya ashindwe kufanya shughuli za kijami.

## 6.0 MAFAO ENDAPO KIFO KITATOKEA

Iwapo mfanyakazi atafariki kutokana na ajali au ugonjwa unaotokana na kazi: Malipo hutolewa kwa mjane, mgane au watoto wa mfanyakazi atakayefariki kutokana na ajali au ugonjwa uliotokana na kazi. Endapo hakuna mjane, mgane au watoto, malipo yatalipwa kwa ndugu wengine wa marehemu watakaotambulika na Mahakama.

***"Fidia Stahiki kwa Wakati"***

## 7.0 UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA AJALI, UGONJWA/KIFO

a) Mfanyakazi au mtu yeyote kwa niaba ya mfanyakazi aliyepata ajali/kifo au ugonjwa unaotokana na kazi, ana wajibu wa kutoa taarifa kwenye Ofisi za Utawala, Mratibu wa Usalama Mahala pa Kazi (OHS) au Ofisi za WCF ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi tokea madhila yalipotokea.

14 SIKU

b) Mwajiri atalazimika kuwasilisha taarifa za ajali au ugonjwa unaotokana na kazi kwa njia ya kielektroniki kupitia portal.wcf.go.tz ndani ya siku saba (07) tokea tukio lilipotokea. Aidha, madai ya ajali, ugonjwa au kifo kinachotokana na kazi yanapaswa kuripotiwa WCF ndani ya kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili (12). Endapo mwajiri au mfanyakazi aliyepata madhila atachelewa kuwasilisha madai kwa kipindi cha miezi kumi na mbili (12) atapoteza vigezo vya kulipwa fidia chini ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura 263 [marejeo ya mwaka 2015].

12 MIEZI

## 8.0 UWASILISHAJI WA NYARAKA

a) Mwajiri atalazimika kuwasilisha nyaraka zifuatazo kupitia *portal.wcf.go.tz*

### AJALI

a) Nakala ya Mkataba wa kazi au barua ya ajira.
b) Ripoti ya tukio la ajali kazini.
c) Fomu ya Madai (WCC 1).
d) Ripoti ya Polisi ikiwa ajali imetokea nje ya eneo la kazi ikihusisha chombo cha moto au jinai.

### UGONJWA

a) Nakala ya Mkataba wa kazi au barua ya ajira.
b) Ripoti ya uchunguzi kutoka kwa Daktari.
c) Fomu ya Madai (WCC 1).
d) Ripoti ya Polisi ikiwa ajali imetokea nje ya eneo la kazi ikihusisha chombo cha moto au jinai.

### KIFO

a) Nakala ya Mkataba wa kazi au barua ya ajira.
b) Ripoti ya tukio la ajali kazini.
c) Nakala ya Cheti cha Kifo.
d) Nakala ya Kibali cha Mazishi.
e) Fomu ya Madai (WCC 1).
f) Ripoti ya Polisi ikiwa ajali imetokea nje ya eneo la kazi ikihusisha chombo cha moto au jinai.

b) WCF itamtaarifu mwajiri na mfanyakazi kuhusu kukubaliwa au kukataliwa kwa taarifa ya tukio la ajali, ugonjwa au kifo baada ya uhakiki.

c) Mwajiriwa ambaye taarifa yake ya tukio la ajali imekubalika ataendelea na hatua ya uwasilishaji wa fomu za matibabu au nyaraka za mirathi:

### FOMU ZA WCF ZA MATIBABU
(mgonjwa anayeendelea na matibabu)

a) Ripoti ya awali ya matibabu (WCC-2A).
b) Ripoti ya maendeleo ya matibabu (WCP – 3) – Ijazwe kila mgonjwa anapoenda kliniki.
c) Taarifa za Mfanyakazi za Kibenki.

### FOMU ZA WCF ZA MATIBABU
(mgonjwa anayeendelea na matibabu)

a) Ripoti ya awali ya matibabu (WCC-2A).
b) Ripoti ya maendeleo ya matibabu (WCP – 3).
c) Ripoti ya Mwisho ya matibabu (WCC-2B).
d) Taarifa za Mfanyakazi za Kibenki.

### NYARAKA MIRATHI

a) Kiapo cha Msimamizi wa Mirathi.
b) Hukumu ya Mahakama.
c) Nakala ya Muhtasari wa Kikao cha Familia.
d) Nakala ya Cheti cha Ndoa (kama kuna mjane/mgane).
e) Nakala ya Vyeti vya Watoto (kama kuna watoto).
f) Fomu ya Wategemezi (WCP 7).
g) Taarifa za benki za wategemezi.

## 9.0 USHUGHULIKIAJI WA MADAI WCF NA KUPATA UFAFANUZI

WCF itashughulikia madai yatakayowasilishwa na kukamilika nyaraka zote zinazohitajika ndani ya siku 30 na kutoa majibu kwa njia ya barua kwa mwajiri na mfanyakazi ya namna fidia ilivyokokotolewa kwa kulipwa. Barua zote zitakazotolewa na WCF zitapatikana katika mfumo wa portal.wcf.go.tz. WCF ina wajibu wa kutoa ufafanuzi wa madai yatakayowasiishwa pale itakapohitajika.

## 10.0 KINGA DHIDI YA UNYANYASAJI

Mfanyakazi hatakiwi kutishwa, kubughudhiwa, kuadhibiwa au kubaguliwa kwa sababu ya kudai au kutaka kudai fidia. WCF.

***"Fidia Stahiki kwa wakati"***

# HAPPY CORNER



# HABARI KATIKA PICHA




















WCF
Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED


Jarida hili limeandaliwa na
Kitengo cha Uhusiano kwa Umma:
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)


Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 3,
S.L.P 329, 41104 Dodoma,
TANZANIA